kuvutiwa na sera za ...

# Wavuvi 74 wapatikana wakiwa hai

**Mwandishi Wetu,** Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Pemba.** Wavuvi 74 wa Shehia za Micheweni Pemba, waliokuwa katika chombo kimoja cha uvuvi na kuzama, wamepatikana wakiwa hai.

Akizungumza na wavuvi hao baada ya kufika bandarini, Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Salama Mbarouk Khatibu alisema ushirikiano baina ya jamii na Serikali, ndio chanzo cha kuwapata wavuvi hao wakiwa hai.

Alisema ni vyema wavuvi wanapokwenda baharini wajuane ili ikitokea hitifafu ya aina yoyote ifahamike.

"Wilaya yetu tumejipanga kuona majanga yote ambayo yatajitokeza tunapambana nayo, ili mambo yote yawe sawa na kila mwananchi ameona matunda ya Serikali hii," alisema Khatibu.

Mmoja wa wavuvi hao, Hamad Omari alisema upepo mkali na mawimbi mazito ndio chanzo cha kuzama kwa boti waliokuwa wakivulia.

wa

NA
Ma
ma
ku



KU
HABAR
N

UHURU UK 10.

# Wavuvi 74 waliodhaniwa kuzama majini wapatikana wakiwa hai

WAVUVI 74 wa Shehia za Micheweni, Pemba, waliokuwa katika chombo kimoja cha uvuvi, ambao awali walihofiwa kuzama wakati wakiwa kwenye harakati za uvuvi, wamepatikana wakiwa hai.

Akizungumza na wavuvi hao baada ya chombo chao kufika bandarini, Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Salama Mbarouk Khatibu, alisema ushirikiano baina ya wanajamii na serikali, ndio uliowezesha wavuvi hao kupatikana wakiwa hai.

Alisema ushirikiano huo ni wa kutoa taarifa haraka uliofanywa na jamii, kisha serikali ya wilaya kwa kushirikiana na vikosi vyake mbalimbali, iliingia kazini kuanza kuwatafuta.

Alieleza kuwa ni vyema wavuvi wanapokwenda baharini, kupeana taarifa ili likitokea tatizo au dosari ya aina yoyote, waweze kutambulika pamoja na chombo walichotumia.

> **"Wilaya yetu tumejipanga kuona majanga yote yatakayojitokeza tunapambana nayo ili kuona mambo yawe sawa na kila mwanachi ameona matunda ya serikali hii.**
>
> Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Salama Mbarouk Khatibu

"Wilaya yetu tumejipanga kuona majanga yote yatakayojitokeza tunapambana nayo ili kuona mambo yawe sawa na kila mwanachi ameona matunda ya serikali hii," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Hamad Mbwana Shehe, alisema amekuwa msatari wa mbele kuwasaidia wavuvi pindi wanapokumbwa na majanga wakiwa katika shughuli zao za uvuvi.

Alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa wavuvi juu ya kufuatilia utabiri wa hali ya hewa ili kujua kama kutakuwa na viashiria vya hatari wasiende kwenye shughuli zao kwa siku hiyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Kukabiliana na Maafa Pemba, Khamis Arazaki Khamis, alisema wamekuwa karibu mno na wananchi wote waliopo Pemba, kutoa elimu na msaada wanapokumbwa na majanga.

Mmoja kati ya wavuvi waliopatikana wakiwa hai, Hamad Omari, alisema upepo mkali na mawimbi mazito ndio chanzo cha kuzama kwa boti waliyokuwa wakivulia.

Alisema upepo huo ghafla ulikiathiri chombo chao na kwamba, walipoondoka bandarini, hakukuwa na dalili za kuwepo kwa upepo mkali.

Julai 25

Ma
ku

WANA
miw
wan
wingi katik
walivyojiandi
kuchukua vi
kura ili kuj
ya uchaguz
kufanyika Ok
Imeelezw
lilikwenda v
utulivu mkul
vitambulisho
utaratibu m
mmoja kup
usumbufu.
Makamu
Uchaguzi Z
Jabu Makar
wakati akiz
wa habari k
vitambulish
Shule ya Ch
Alisema
vilitolewa k
kupunguza
kwamba kw
kwenye kit
vituo vya T
kila wilaya.
"Tume

MAONI



Mba

JESHI la Poli
Unguja, linar
(32), mkazi
kujifanya ofi
la kuwatapel
Akitoa ta
jana, kuhus
mkoa huo,
huo, Awadh
anatuhumiw
mwaka huu
Msingi Mne
Alisema
ya jeshi hi
akiyafanya
kuwadanga
katika Idar
nyingine z
na Vitu, tof